

**Dondoo za mkutano wa Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam**  
**26 Aprili 2008**

**Waliohudhuria**

Ally Athuman Jumbe  
Ally Saidi Mohamedi  
Aseli Wilison  
Elaine Baker  
Filbert Mbecha  
Juma Ali Salehe Jongo  
Jumanne Idd Selemani  
Markus Weise  
Musa Athumani Lahi  
Mussa Alex  
Rahma Ali  
Sudi Saidi Ramadhan

**Uzinduzi wa ofisi**

Jumamosi wiki jana tulisherehe uzinduzi wa ofisi yetu. Wageni waliohudhuria:

- Leonard Lupilya, diwani ya Mchikichini kwenye Halmashauri ya Manispaa ya Ilala
- Kassim Lema diwani ya kata ya Mabibo
- Mihayo Ilembompria mwenyekiti wa mtaa
- Walukani Luhamba afisa mfawidhi wa kanda ya mashiriki SUMATRA
- Madaba B.S. wa SUMATRA
- Benedict Kaguo kutoka gazeti ya Majira
- Peter S Makelemo wa ATD fourth world
- Salehe M Seif wa ATD fourth world
- Saidi Kengelle kutoka CHABADA

Azzan Zungu MP hakuweza kuhudhuria kwa sababu alikuwepo bungeni lakini alitutumia ujumbe kututakia kila ya heri. Wageni wote walitupa hongera ya malengo na mafanyikio yetu. Tulitoa helmeti, t-shirt na jaketi ya njano kwa wanachama waliohudhuria mikutano na pia uzinduzi na pia tulitoa t-shirt na helmet moja kwa wageni. Helmeti tatu na jaketi za njao mbili zinabaki.

Ally Saidi Mwishehe, Ally Athman na Juma walisafirisha hema, Dominata alikuwa MC na Sosthenes, Mejah na Elaine walitoa hotuba. Kila mgeni alijitambulisha na alichangia mawazo.

**Ofisi**

Sudi Saidi alipendekeza tupake rangi ya aina za baisikeli zote tatu (guta, ya walemvu na ya kawaida) kwenye milango ya ofisi. Wanachama wengine walipendekeza tupate meza na viti.

### **Mambo ya hela**

Tulilipa Tsh 10,000 ya ziada ya kukodi vifaa vya muziki (pamoja na advance ya Tsh 20,000), Tsh 30,000 kwa ajili ya hemu, Tsh 19,500 kwa ajili ya sodas na Tsh 5,000 kwa ajili ya umeme. Tulipata mchango wa Tsh 10,000 kutoka Bwana Kassim Lema. Elaine alirudishwa hela yake ya Tsh 25,000 alitumia kwa faili na advance na Mejah alirudishwa hela yake ya Tsh 10,000 alitumia kwa ajili ya vifaa vya kutengeneza alama za kuonyesha nji kwenda ofisini. Juma alirudisha Tsh 50,000 kwenye benki kutoka Tsh 150,000 yeye na Mejah walichukua kutoka benki kabla ya uzinduzi. Juma anabaki na Tsh 14,000 ya hela ya UWABA. Jumanne alitupa lino kwa uzinduzi wa ofisi na wanachama walikubali kununua kabisa, basi Juma atampa Jumanne Tsh 10,000.

### **Utambulisho wa Markus**

Markus Weise alifika Tanzania jumanne atakaa hapa miezi miwili kusaidia katika shughuli za UWABA. Alijitambulisha na alisema yupo kwenye Watson Fellowship scheme. Amekaa Namibia, Bangladesh na Vietnam chini ya scheme hiyo na alituonyesha picha za baisikeli za kule. Wanachama walimwuliza maswali na tulibadalisha mawazo.

### **Mradi wa Usalama Barabarani - Wamba Memorial Fund**

Dr Osili kutoka Wamba Memorial Fund alisema kwamba wametuma hela ya \$3,000 kwenye akaunti ya UWABA jumatatu iliyopita, lakini Juma alipoenda benki ijumaa hela bado haijafika. Ataangalia tena wiki ijayo pamoja na namba ya kumbokumbo. Pia Dr Osili alisema kwamba Elaine Wamba atakuu Tanzania mwaka huu kutana nasi.

Tulikubali tutashirikiana na Chuo cha Taifa cha Usafirishaji katika mradi wa usalama barabarani kwa sababu walishirikiana nasi katika semina, wana wataalamu wa usalama barabarani, wana uwanja na wanaweza kuwa na vifaa kama pembe tatu kwa ajili ya vitendo. Tulikubali Elaine atanadika barua kuomba mkutano nao kuhusu mradi huu na Juma na Markus wataenda na barua kuongea nao.

Kwenye uzinduzi Bwana Lupilya alisema atafahamu shule ipo Msongola manispaa ya Ilala ambapo wanafunzi wengi wanaenda shulenii na baisikeli. Tulikubali tutaomba namba ya simu za walimu wa shule hii ili tuwaombe kushirikiana katika mradi. Ally Athman alisema kwamba naibu Waziri wa Miundombinu Bwana Makongoro Mahanga pia ni mbunge wa Ukongo ambapo shule hii ipo basi tunaweza kuwasiliana naye pia.

Tulikubali Juma na Markus watatembela HUWATA kuwaambia kwamba mradi unaanza.

### **Traffic police**

Bado hatujapata jibu la barua yetu kuomba mkutano na traffic police. Juma na Markus watambelea ofisi zao kufuatalia.

### **Mwanachama mpya**

Mussa Alex ana miaka 10, yupo darasa la tatu, na anaenda kutoka Mabibo mpaka shulenii Sinza kila siku na baisikeli. Wanachama walimpa hongera na tulikubali kumpatia helmeti.

### **TANROADS na Morogoro Road**

Hatujapata jibu la barua letu kwenda TANROADS kuhusu swala la vifereji barabara ya Morogoro maeneo ya Jangwani. Juma na Markus watafuatalia wiki hii.